# ALLIANCE HIGH SCHOOL

## KCSE

## MTIHANI WA KISWAHILI

**INSHA**

**Wewe ni mwenyekiti wa Kamati ya Dharura ya kushughulikia janga la Korona. Mwandikie barua mhariri wa Gazeti la Pilipili ukieleza athari za janga hili kwa jamii nzima.** (Alama 20)

**Athari hasi:**

i. *Kupoteza kazi/Biashara/Njia za kupata mapato.*
ii. *Hospitali kufurika.*
iii. *Watu kuogopa kwenda hospitalini ili kutibiwa magonjwa mengine.*
iv. *Fedha nyingi kutumiwa kukabiliana na janga hili.*
v. *Unyanyapaa kwa walioambukizwa.*
vi. *Mfumko wa bei za bidhaa na huduma muhimu.*
vii. *Kupigwa marufuku kwa mikutano ya halaiki k.m. kanisani.*
viii. *Kuhitilafiwa kwa kalenda ya masomo.*
ix. *Vifo (watu na wahudumu wa afya).*
x. *Hofu miongoni mwa wanajamii.*
xi. *Kafyu.*
xii. *Msongo wa mawazo.*

xiii. *Kuvunjika kwa familia.*
xiv. *Kusambaratika kwa mahusiano.*
xv. *Usafiri baina ya nchi moja na nyingine.*
xvi. *Mimba miongoni mwa watoto.*
xvii. *Mila potovu k.v. Ukeketaji, mila potovu.*
xviii. *Matumizi zaidi ya madawa za kuolevya.*
xix. *Thamana ya shilingi kushuka.*
xx. *Hadhi ya binadamu kushuka katika mazishi.*
xxi. *Kuwepo kwa karantini.*
xxii. *Kuongezeka kwa ulaghai na ufisadi.*
xxiii. *Kuzidi kwa kuchakura mitandao ya pomografia/filamu mbaya.*

**Athari chanya**

xxiv. *Baadhi ya biashara zilinawiri k.v. uuzaji wa barakoa, vieuzi na mitandao kama Zoom.*

**UFAHAMU**

a) **Huku ukirejelea kifungu, fafanua <u>faida sita</u> utakazopata ukiishi shambani.** **(Alama 6)**

i. *Kufurahia na kunufaika na mazingira (mandhari) ya kijani kibichi yanayopendeza hadi upeo wa macho na sauti za ndege zinazoburudisha na kuliwaza.*
ii. *Ushirikiano au utangamano kati ya babu na wajukuu wake na hata kati ya wanakiji mbao hujaliana maslahi na kukuza ukarimu kwa kusaídiana na kuombana vyakula kama vile unga na mboga.*

iii. *Kunufaika kutokana na ubora wa vyakula vya kiasili kama kuku wa kiasili ambaye huwa na ladha ya kupendeza na pia huwa mgumu kiasi cha kuwasaidia watu (Wanakijji)kuimarisha meno.*

iv. *Shambani hamna misongamano barabarani kwa hivyo mtu huweza kutekeleza shughuli zake mbalimbali wakati wowote anapotaka bila vizuizi.*

v. *Kujuana. Kijjini watu hujuana, huamkuana kila siku, hujuliana hali na hata kula pamoja ilhali mjini hata majirani hawajuani.*

vi. *Usalama barabarani kwa sababu shambani hamna barabara kubwa na pana au 'haibei' zinazosababisha ajali nyingi au hata vifo vingi vya watu kama ilivyokuwa kwa jirani ya babu yake msimulizi.*

vii. *Kuepuka uzembe kwa kufanya kazi za sulubu (ngumu) ili kuufanyisha mwili mazoezi.*

viii. *Kuwa na afya nzuri kutokana na kula vyakula halisi vya kienyeji (kiasili) vilivyo na faida nyingi mwilini hivyo kuepuka udhaifu na magonjwa yatokanayo na ulaji wa chakula hafifu kama kuku wa miigizo walio na faida duni kwa mwili.yotakikanaKutambua asili au usuli hivyo kuwa na mizizi imara ya kutosha.*

*Tanbihi: Toa majibu sita pekee kama ulivyoagizwa.*

**b) Eleza <u>mtazamo wa wahusika</u> wafuatao kuhusu mji:**

**Msimulizi** **(Alama 3)**

i. *Mjini mna raha na maendeleo yanayoashiriwa na wingi wa magari.*

ii. *Uwezo wa kifedha wa watu wa mjini uko juu kuliko wa kijijini.*

iii. *Wanaoishi mjini hupata huduma za dharura kwa urahisi kama vile mgonjwa huweza kuhudumiwa haraka ipasavyo.*

iv. *Usafiri upo kila mahali wakati wowote mjini.*

*Tanbihi: Katika swali hili mtahiniwa hakuambiwa idadi ya majibu inayotakikana. Katika hali kama hii, atoe majibu yote ayaonayo katika ufahamu.*

**Babu** **(Alama 4)**

i. *Mjini hamna ustaarabu ambao wanaoishi mle ndani kuwapo*
ii. *Maisha ya mji yeye kasi isiyoridhisha na utulivu haupo*
iii. *Kutojuana: mjini jamaa hata majirani hawajuani, hawaamkuani,hawasaidiani wala hawashirikiani katika mlo.*
iv. *Mji hufanya watu kutotambua asili yao hivyo kukosa mizizi thabiti.*
v. *Mji huteteresha mahusiano ya kijamii wanajamii wanapokosa kujaliana.*
vi. *Mji hupalilia uzembe na watu kutoushughulisha mwili.*
vii. *Mji hutinga utekelezaji wa shughuli kwa sababu ya msongamano barabarani-watu kupoteza muda.*
viii. *Vyakula vya mjini kama vile kuku wa miigizo vina faida duni mwilini*
ix. *Mjini barabara ni hatari*
x. *Watu wa mji hawana siha nzuri kutokana na vyakula duni wanavyokula.*

c) **Andika maana ya fungu lifuatalo la maneno kwa mujibu wa taarifa:** **(Alama 1)**

**kwenda kwa wakwe wako upate ndio wanakwenda uchi.**

*Kwenda kwa mtu na kumpata ndipo anapofanya kosa / hajajitayarisha / yuko katika hali ya aibu au fedhaha.*

d) **Andika kisawe cha:** **(Alama1)**
**Niliona kisunzi :** *Kuhisi kizunguzungu / Kisulisuli.*

**MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 20)**

**a) Taja sauti moja ambayo ni:** **(Alama 1)**

**Kituo ghuna cha midomo.** */b/*

**King'ong'o cha kaakaa gumu.** */ny/*


**b) Ainisha viambishi katika kitenzi.** **(Alama 1)**

**Waliowaandalia**

*Wa-li-o-wa – Viambishi awali*

*-li-a – Viambishi tamati*

**c) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mchoro wa matawi. (Alama 2 ½)**




**d) Tambua aina za shamirisho katika sentensi hii.** **(Alama 1 ½)**

**Busara alimbebea mzazi wake mzigo kwa gari.**

*Kipozi - mzigo*

*Kitondo – mzazi wake*

*Ala – gari.*

**e) Unda nomino moja inayorejelea kitendo kutokana na kitenzi.(Alama 1 )**

**Cheza -** *mchezo*

**f) Andika kwa usemi wa taarifa.** **(Alama 1)**

**"Mbona ulimfanyia mzazi ujeuri? Je, utaenda kumwomba radhi?" Nasaha alimwuliza Katili.**

*Nasaha alimwuliza Katili kwa nini alimfanyia mzazi ujeuri na kutaka kujua iwapo angeenda kumwomba radhi.*

**g) Eleza matumizi ya 'na' katika sentensi hii. (Alama 1)**

**Mwanafunzi anayesoma vizuri alielekezwa na mwalimu wake.**

*Anayesoma – wakati uliopo*

*na - mtendaji*

**h) Andika wingi wa ukubwa wa sentensi hii. (Alama 1)**

**Mbuzi alipigwa kwa jiti akatoroka.**

*Mabuzi yalipigwa kwa majiti yakatoroka.*

**i) Andika sentensi mojamoja kuonyesha matumizi ya: (Alama 1)**

**Kinyota (*)**

1. *Kuashiria neno lina kosa la tahajia/hijai mf. babe* badala ya baba.*
2. *Kuashiria neno linahitaji uzingatifu mfano Bosibori* ndiye mshindi.*
3. *Kuonyesha neno ambalo litaelezewa zaidi chini ya ukurasa.*
   *Mf. Alipopata nafasi ya kuingia shule ya upili ya Alliance*, mwanafunzi huyo alijawa na furaha tele.*

   ---

   **Alliance ni mojawapo ya shule zinazofanya vizuri zaidi barani Afrika.*

   **Uk 100.**
4. *Kuficha herufi/silabi katika neno ili kupunguza ukali wa maneno yasiyo na nidhamu. Mf: Rais aliwaita wananchi m**i ya kuku.*
   *Aidha, alisema kwamba nyote ni wapu***vu.*

**Kibainishi/Ritifaa (')**

1. *Hutumika kutofautisha sauti /ng'/ na /ng/ Ngoma ile inang'ang'aniwa.*
   *Ng'ombe wote wanang'ang'aniwa.*
2. *Kuandika maneno kwa kifupi kwa mfano; S'endi (sauti /i/ imetolewa)*
3. *Huonyesha herufi iliyoachwa mf Alifanya kazi kutoka 1968-199'.*

**j) Nomino 'mijusi' iko katika ngeli gani ?** *A-WA* **. (Alama ½ )**

**k) Yakinisha sentensi hii. (Alama 1 )**

**Sitaandika insha murwa na mufti leo.**

*Nitaandika insha murwa leo.*

l) **Onyesha <u>vishazi</u> katika sentensi hii.** **(Alama 1)**

**Mwanafunzi hodari aliyepita mtihani amesifiwa.**

*Mwanafunzi hodari aliyepita mtihani – kishazi tegemezi*

*Mwanafunzi amesifiwa – kishazi huru*

m) **Tambua <u>kijalizo</u> katika sentensi hii.** **(Alama 1)**

**Mgeni aliyefika jana jioni ni mtaalam.** *Mtaalam*

n) **Onyesha <u>virai</u> katika sentensi hii huku ukieleza ni vya <u>aina gani</u>.**

**Maria anapenda kusoma vitabu vyenye mvuto halisi.** **(Alama 1)**

*anapenda kusoma – kirai kitenzi*

*vitabu vyenye mvuto halisi – kirai nomino*

o) **Kwa kutolea <u>mfano faafu tofautisha</u> kati ya <u>kiima</u> na <u>kiarifa</u>. (Alama 2)**

*Kiima/Kundi nomino - Sehemu ya sentensi yenye nomino/neno kuu ni nomino. Mf Mwalimu anafunza.*

*Kiarifa/kundi tenzi - sehemu ya sentensi yenye kitenzi/ neno kuu ni kitenzi. Mf Mwanafunzi anasoma.*

p) **Andika sentensi hii upya ukitumia <u>vinyume</u> vya maneno <u>yaliyopigiwa mstari</u>.** **(Alama 1)**

**Kazana amefaulu <u>kuhifadhi</u> pesa zake, kwa hivyo <u>ametajirika.</u>**

*Kazana amefaulu <u>kufuja</u> pesa zake, kwa hivyo <u>amefilisika.</u>*

q) **Andika sentensi hii katika <u>hali isiyodhihirika</u>.** **(Alama ½ )**

**Alianguka akicheza.** *Aanguka akicheza*.

r) **Tunga <u>sentensi ya neno moja</u> yenye <u>visehemu hivi vya sarufi</u>. (Alama 1)**

**Kiambishi kiwakilishi cha kiima.**

**Kiambishi kiwakilishi cha wakati ujao.**

**Kiambishi kiwakilishi cha mtendewa.**

**Mzizi.**

**Kiambishi cha kauli ya kutendesha.**

**Kiishio**

*Atamsomesha, alikichezesha n.k*

**UFUPISHO**

a) **Fupisha ujumbe wa aya tatu za mwanzo kwa maneno 85-90. (Alama 5)**

i. *Katiba mpya iliidhinisha mfumo wa ugatuzi ambao hupunguza mamlaka ya serikali kuu katika usimamizi wa rasilimali*
ii. *Eneo la ugatuzi hutwaa kiasi fulani cha mamlaka.*
iii. *Ugatuzi utahakikisha usawa wa kimaendeleo nchini kinyume na awali.*
iv. *Serikali isaidie maeneo yote kujiimarisha.*
v. *Maeneo yaweke mikakati ya kutafiti na kubainisha rasilimali/zilizomo.*
vi. *Kuvumbua rasilimali mwafaka kutasaidia ustawi.*
vii. *Wanamaeneo watafute mbinu za kuongezea thamani rasilimali.*
viii. *Kilimo cha ufugaji ni nguzo ya maeneo mengi na kinahitaji kuimarishwa kwa kuandama*
ix. *Mbinu za kisasa za uzalishaji.*
x. *Ipo haja ya wananeneo kukabiliana na matatizo yanayohusiana na soko ili kukinga dhidi ya kupoteza wateja.*
xi. *Ipo haja ya kujenga viwanda vya kuchinjia mifugo na kupakia nyama.*
xii. *Baadhi ya wafugaji huhasirika kwa kuuza mifugo.*

xiii. *Wafugaji wengine hutapeliwa.*

**Jibu:**

**b) Kwa kutumia maneno 75-80, bainisha masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tatu za mwisho. (Alama 5)**

i. *Ujenzi wa viwanda vya kuchinjia na kupakia nyama utakinga dhidi ya kupoteza bidhaa zinazotokana na mifugozinazotokana na mifugo.*
ii. *Kujenga viwanda hivi kunasababisha ujenzi wa viwanda tegemezi.*
iii. *Hili litawezesha kuzalisha nafasi za kazi.*
iv. *Kutakuwa na kuongezea thamani utoaji wa huduma za kijamii na kiutawala.*
v. *Kuzalisha nafasi za kazi kwa vijana kutasaidia kuwaadilisha vijana zaidi.*
vi. *Kila eneo lina vipaumbele tofauti; wakazi wabainishe kipaumbele chao.*
vii. *Ugatuzi unahitaji ushirikiano.kila mwanaeneo awajibikie maendeleo ya eneo.*
viii. *Wanaeneo washiriki kuteua viongozi wenye muono mzuri.*
ix. *Ufanisi katika maeneo ya ugatuzi utachangia katika ufanisi wa taifa kwa jumla.*

**ISIMUJAMII**

**Fafanua maana ya istilahi zifuatazo. (Alama 10)**

**Viziada Lugha:** *Viongezi katika matamshi kama makofi, ishara za mikono n.k*

**Kaida za Lugha**: *Sheria zinazotawala matumizi ya lugha kama vile: Mazingira/mahali, Jinsia/uana, cheo/hadhi, umri, mada, muktadha, wakati/misimu, Malezi, Taaluma/kazi/shughuli, Mila/desturi/utamaduni, Hadhira/.Njia ya mawasiliano, imani/dini/itikadi, Tajriba/uzoefu/ujuzi, Elimu(kiwango cha elimu), Hali/hisia.*

**Kubadili msimbo:** *Kubadili lugha katika mazungumzo. Sentensi moja katika lugha fulani kisha sentensi inayofuata katika lugha tofauti.*

**Sifa bia za Lugha:** *Tabia zinazofanana katika lugha yoyote ile kama: Hakuna lugha iliyo bora kushinda nyingine - zote ni sawa, Kila lugha ina sauti zake zilizo tofauti na zingine, Lugha hubadilika kutegemea mazingira, aina ya tukio, wakati na watumizi wa lugha hiyo, Lugha ina uwezo wa kuzaliwa, kukua, lugha pia huweza kufa huku msamiati wake kupotea kabisa.*

**Pijini:** *Lugha iliyoibuliwa kutokana na msamiati, sauti na ishara zilizokopwa na imerahisishwa huku ikitumiwa kuwaunganisha wazungumzaji wenye lugha tofauti.*

**Lingua franka:** *Lugha moja inayozungumzwa pahali palipo na wingi lugha ili kurahisisha mawasiliano.*

**Lahaja:** *Tofauti za kimatamshi, maumbo na matumizi ya maneno katika maeneo mbalimbali kwa lugha yenye asili moja, vijilugha katika lugha moja kuu.*

**Sajili:** *Rejesta au matumizi ya lugha kulingana na muktadha wa matumizi yake.*

**Maenezi ya Kiswahili:** *Kusambaa kwa Kiswahili.*

**Wingi lugha:** *Uwezo wa kuongea lugha nyingi.*

**FASIHI SIMULIZI**

**Fafanua vipera vifuatavyo: (Alama 10)**

**Ngomezi:** *Fasihi ya ngoma / matumizi ya ngoma au ala kuwasilisha ujumbe badala ya kutumia maneno. Aghalabu ujumbe tofauti huwasilishwa.*

**Mivigha/Miviga:** *Sherehe maalum za kitamaduni ambazo hufanywa na jamii yoyote katika kipindi maalum cha mwaka na aghalabu huambatanishwa na nyimbo, kama vile: tohara, unyagoni, jandoni, arusi za kitamaduni, mazishi, kuingizwa katika rika,*

*kutawazwa kwa viongozi wa kitamaduni, kupunga mapepo, maombi kabla ya vita, watoto kupewa majina, kuanza ujenzi, n.k.*

**Maapizo:** *Maombi ya kumlaani mtu/ Maombi maalumu ya kumtakia Mungu / mizimu kumwadhibu mhusika mwovu.*

**Matambiko:** *Sadaka inayotelewa kwa Mungu / miungu ili kutoa shukrani au kuomba radhi.*

**Ngano za mtanziko:** *Hadithi ambazo mhusika hujipata katika njia panda.*

**Soga:** *Mazungumzo / masimulizi ya kupisha wakati / hadithi fupifupi zinazosheheni utani na ucheshi fulani na hukusudiwa kutoa funzo fulani.*

**Hodiya:** *Nyimbo za kazi.*

**Vivugo/Majigambo:** ***T**ungo za kujisifu zinazoghaniwa na mtu binafsi/ Utungo wa kujisifia unaotungwa papo kwa hapo, hasa baada ya ushindi katika harakati ngumu.*

**Misimu:** *Semi zinazozuka katika kundi fulani la watu katika kipindi fulani kisha kutoweka au kuimarika na kukubalika katika lugha fulani. Mfano wa misimu ni maneno ya sheng'*

**Vitanzandimi:** *Maneno yenye kuundwa kwa sauti zinazokaribiana kimatamshi. Mf. Wali huliwa na mwana wa liwali. Asiyekuwa mwana wa liwali hali wali.*

**USHAIRI**

a) **Eleza hali ya mzungumziwa katika shairi hili. (Alama 1)**

*Mcheshi, Mwenye bidi au Maskini .*

b) **Huku ukitoa mifano, onyesha aina mbili za uhuru wa kishairi uliotumiwa katika shairi hili (Alama 2)**

*Inkisari; babuze – babu zetu*

*Kuboronga sarufi; Aliye na kubwa hamu*

*Aliye na hamu kubwa*

c) **Fafanua aina tatu za taswira ukirejelea ubeti wa pili (Alama 3)**

*Taswira sikivu, anasikiliza videge vya anga vinavyotumbuiza*

*Taswira mnuso; Rihi ya maua zikimletea*

*Taswira mguso; umande kumbusu miguuni*

d) **Maswali ya balagha katika shairi hili yanasisitiza maudhui yapi? (Alama 2)**

*Unyanyasaji*

*Kunyimwa haki kwa binadamu maskini*

e) **Kwa kutoa mifano, bainisha vipengele vitatu vya Kimtindo katika shairi hili (Alama 3)**

*Tashihisi - umande kumbusu miguuni.*

*Kinaya - kuwa mrejelewa ana furaha ilhali anafanya kazi za sulubu (kulima).*

*Tashibihi - Tabasamu kama mtu aliye na kubwa hamu.*

f) **Eleza toni ya shairi hili (Alama 1)**

*Huruma - mateso mrejelewa anayoyapitia*

g) **Bainisha nafsineni katika shairi hili (Alama 1)**

*Mchunguzi / mpita njia wa karibu na mrejelewa*

h) **Eleza muundo wa shairi hili (Alama 2)**

*Kuna beti*

*Mistari mishata*

*Mishororo haina mizani sawa*

*Hakuna urari wa vina*